**SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAJI**

## WAKALA YA USAMBAZAJI MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (RUWASA)

**Ubungo barabara ya Chuo Kikuu,**
**S. L. P 55658,**
**Dar es Salaam**
**Tanzania**

**Simu:- +255-22-2410299**
**Nukushi:- +255-22-2410384**
**Barua pepe: info@ruwasa.go.tz**
**Tovuti: www.ruwasa.go.tz**

# TAARIFA KWA UMMA

Katibu Mkuu Wizara ya Maji ***Prof. Kitila Mkumbo*** leo tarehe 19 Julai, 2019 amezungumza na wafanyakazi wa iliyokuwa Wakala ya Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) kuhusu mambo mbali mbali ya kiutendaji na kiutumishi yatakavyotekelezwa hasa katika kipindi hiki cha mpito ambapo Wizara imeanzisha Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Awali kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi, Kaimu Mkurugenzi Mkuu (DG) Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mhandisi ***Gonsalves Rutakyamirwa*** alitoa taarifa ya watumishi wa iliyokuwa DDCA pamoja na miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa kama vile mradi wa ujenzi wa bwawa la mbangala ambao umekamilika kwa asilimia 35, Uchimbaji wa visima 12 Kibondo, Ukarabati wa visima 8 Gairo, Mradi wa maji Kirando pamoja na mikataba 24 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Aidha, ***Prof. Kitila Mkumbo*** amesema iliyokuwa DDCA ndiyo mtaji mkubwa wa RUWASA kwa kutoa ufafanuzi na mtazamo wa namna ambavyo utekelezaji wa kazi za uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa utakavyofanyika katika kipindi hiki cha mpito bila kuathiri michakato na taratibu za kisheria za manunuzi ya umma.

Katibu Mkuu amewahimiza wafanyakazi wote kuacha kufanyakazi kwa mazoea badala yake wafanyekazi kwa weledi na ufanisi ili kutatua changamoto za kupata vyanzo vipya vya maji nchini hasa maeneo ya vijijini hali amabayo itasaidia kuleta tija katika kumtua mama ndoo kichwani.

**Kitengo cha Masoko na Mahusiano**
**RUWASA**
**19Julai, 2019**